

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU CHANJO DHIDI YA UGONJWA WA COVID - 19

DODOMA, 15 JULAI 2021

Chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali zimekuwa zikitolewa duniani kote na nchini Tanzania. Chanjo hizi ni muhimu sana katika kudhibiti na kuondoa magonjwa ambayo yamekuwa yakisababisha madhara makubwa na hata vifo. Mpaka sasa, Tanzania imekuwa kinara katika udhibiti wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo na mengine yameshatokomezwa kabisa mfano ndui na baadhi kuondoka kama vile ugonjwa wa kupooza (polio) na pepopunda kwa watoto wachanga.

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na vifaa tiba (TMDA) imekuwa ikijiridhisha juu ya usalama, ufanisi na ubora wa chanjo zote zinazoingizwa nchini. Aidha, Tanzania kupitia TMDA ni nchi ya kwanza barani Afrika kuwa na chombo kilichofikia kiwango cha hali ya juu (maturity level 3) kinachotambuliwa na Shirika la Afya Duniani katika udhibiti wa dawa na vifaa tiba zikiwemo chanjo.

Kufuatia uchambuzi wa kina wa timu ya wataalamu kuhusu chanjo dhidi ya ugonjwa wa COVID – 19, Serikali iliridhia na kuruhusu kuanza kutolewa kwa chanjo dhidi ya ugonjwa huu kwa kuzingatia misingi ya usalama, ufanisi na ubora wa chanjo ambazo zimeruhusiwa kuanza kutumika nchini kutokana na ushahidi wa kutosha wa kisayansi uliopo. Aidha, mpaka sasa tayari chanjo hizi zimeanza kutolewa kwa baadhi ya jumuiya za kimataifa na baadhi ya makundi mbalimbali nchini na mpaka sasa hakujaripotiwa tatizo dhidi ya chanjo hizi.

Mpaka tarehe ya leo, ugonjwa wa COVID – 19 umeathiri watu zaidi ya 188,310, 529 na kusababisha vifo 4,058, 803 duniani kote. Nchini Tanzania tumeshuhudia kupotelewa na ndugu zetu wapendwa kutokana na ugonjwa wa COVID – 19. Hivyo Serikali imeamua kutumia afua zote zenye ushahidi wa kisayansi katika kudhibiti ugonjwa wa COVID – 19 ikiwemo utoaji wa chanjo salama na zenye ufanisi wa kutosha. Ushahidi unaonyesha kwamba, nchi zilizoathirika kwa kiasi kikubwa hapo awali na kuanza kutoa chanjo kwa wananchi wake walio wengi, maambukizi na vifo vimepungua kwa kiwango kikubwa na hivyo kupelekea kuondokana na adha ya kulazwa na matumizi makubwa ya hewa tiba ya Oksijeni na watu kuendelea na shughuli zao kama kawaida.


Aidha, Wizara inawakumbusha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zote dhidi ya ugonjwa wa COVID – 19 zikiwemo unawaji wa mikono kwa maji safi tiririka na sabuni, kutumia vipukusi, kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima, kukaa umbali wa mita moja au zaidi kati ya mtu mmoja na mwingine, uvaaji na matumizi sahihi ya barakoa, ufanyaji wa mazoezi ya mwili na lishe bora ili kuuweka mwili katika hali ya kinga dhidi ya magonjwa na kuendelea kuyalinda makundi yaliyo katika hatari zaidi na kuanza kutoa chanjo.

Chanjo zilizoruhusiwa na Serikali ni zile zilizo rodheshwa na Shirika la Afya Duniani na TMDA kutokana na usalama, ufanisi na ubora ambapo utoaji wake **utakuwa ni wa hiari**. Ifahamike kuwa, uhiari wa utoaji wa chanjo unaenda sambamba na ridhaa (consent) baada ya elimu ya kutosha kutolewa. Aidha katika fomu iliyotolewa kwenye mwongozo wa chanjo ni ya kawaida na itakuwa inafafanuliwa vyema kwa watakaohiari kupata chanjo, hivyo wananchi wasipokee upotoshaji ndio maana imewekwa wazi

Utoaji wa ridhaa (consent) ikiwemo ya maandishi ni suala ambalo limekuwepo na limekuwa likitumika katika maeneo mbalimbali mfano katika tafiti, utoaji wa chanjo na huduma za matibabu ambapo mpokeaji wa huduma hutoa ridhaa ya kupatiwa huduma husika baada ya kupata elimu. Utaratibu wa fomu ya ridhaa unatumika katika nchi nyingi duniani kwenye utoaji huduma za kinga na tiba ikiwemo chanjo ya COVID - 19.

Wizara inawaomba wananchi kupuuza taarifa zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii zenye lengo la kupotosha umma na hivyo kupunguza kasi ya kudhibiti ugonjwa huu. Hivyo basi, Wizara inawaasa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kuiamini Serikali yao kwani ndio yenye dhamana ya kulinda afya ya wananchi.

Imetolewa na



Dkt. Alfello W. Sichahe

MGANGA MKUU WA SERIKALI